# Je, Agano la Kale, Torati Yote na Amri Kumi ni Mamoja?

Leo watu wengi wanatufundisha kwamba Agano la Kale, Torati na Amri Kumi, ni sheria tofauti. Lakini kama tutachunguza Biblia tunaweza kuthibitisha kwamba **Amri Kumi zinaitwa kuwa ni Agano la Kale, na kwamba Agano la Kale linaitwa pia Torati.**

### Je, Amri Kumi na Agano La Kale ni Moja?

Kwanza tukumbuke maana ya neno "agano" maana yake ni "mapatano" kati ya watu. Ndani ya agano Mungu alivyofanya na Waisraeli, aliahidi kuwapa nchi ya Kanaani na kuwabariki ikiwa watazishika sheria walizopewa mlimani Sinai. Kwa hiyo, sheria zile zilikuwa ndilo agano. Tusoma, "Bwana akasema nanyi kutoka kati ya moto; mkasikia sauti ya maneno, lakini hamkuona umbo lo lote; sauti tu. Akawahubiri agano lake, alilowaamuru kulitenda, yaani, zile amri kumi; akaziandika juu ya mbao mbili za mawe," Kum. 4:12-13. "Bwana akamwambia Musa, andika maneno haya; kwa kuwa mimi nimefanya agano nawe, na pamoja na Israeli kwa mujibu wa maneno haya....Naye akaandika katika hizo mbao, hayo **maneno ya maagano, hizo amri kumi**," Kut. 34:27, 28. Na zile mbao mbili za mawe za amri kumi zilitiwa ndani ya sanduku lililotenganzwa kwa ajili yao (Kumb. 10:1-5). Basi, kwa sababu **amri kumi** zilikuwa **ndilo agano,** ndiyo maana sanduka liliitwa "**SANDUKA LA AGANO."** Musa alisema, "Naye (Mungu) akaandika juu ya mbao mfano wa maandiko ya kwanza, zile amri kumi, alizowaambia Bwana huko mlimani toka kati ya moto siku ya mkutano; Bwana akanipa. Basi nikageuka nikashuka kutoka mlimani, **nikazitia mbao ndani ya sanduku nililofanya;** nazo zimo humo kama alivyoniamuru Bwana....Na wakati huo Bwana aliitenga kabila ya Lawi ili walichukue lile **sanduka la agano la Bwana,**" Kumb. 10:4, 5, 8.

Kwa hiyo tumeona maandiko matakatifu. Na tumeona katika maandiko kwamba **agano la Mungu** (Kumb. 4:12-13) ni **zile amri kumi**. Haya ndiyo maneno ya Biblia. Na katika Kut. 34:27-28, Bwana alimwambia Musa andika maneno haya, maneno gani? Angalia mst. wa 27 na 28 na utapata jibu, "**maneno ya maagano, hizo amri kumi**." Na zile amri kumi ambazo Mungu alivyofanya alimwambia Musa aweka zile sheria katika "Sanduku la Agano la Bwana." Sio sandukua la amri kumi. Lakini amri kumi Musa aliweka katika sunduka la agano! (Kumb. 10:4, 5, 8). Bila shaka tunaelewa ambacho tunasoma, agano la Mungu (Kati ya wana Waisraeli, "Agano la Kale") na amri kumi ni kitu kimoja! (Kumb. 4:12-13).

### Je, Torati na Agano la Kale ni Moja?

Baada ya mapigo kumi Mungu aliongoza Waisraeli kutoka Misri mpaka Mlima Sinai. Walipofika Sinai Mungu alianza kuongea na watu wote wa Israel na kuwapa sheria zake kwa midomo yake mwenyewe. Na Mungu alikuwa na sheria nyingi sana ambazo alitaka kuwambia watu wake wa taifa la Israeli. Lakini kabla ya kumaliza sheria zake, alimaliza **kumi tu** kwa midomo yake, wana wa Israeli walikuwa na hofu sana. Kwa hiyo kwasababu waliogopa sana walimkatisha Mungu na kusema, "Sema nasi wewe, nasi tutasikia, bali Mungu asiseme nasi, tusije tukafa," Kut. 20:29. Kwa sababu ya ombi ya watoto wake (Wana Waisraeli) Mungu alimwita Musa apande Mlima Sinai. Kule

mlimani Mungu alirudia kutoa au kumpa Musa zile amri kumi pamoja na sheria za torati zote zilizobaki wakati alipokatishwa na watoto wake. Na kwa sababu wana wa Israeli walisikia zile amri kumi kwa masikio yao toka kwa sauti ya Mungu, basi Mungu aliandika kwenye mbao mbili zile amri kumi wana Waisraeli waliposikia kutoka katika mdomo wake. Na zile mbao mbili zilikuwa **ushuhuda** juu ya Waisraeli. Tuangalia, Kut. 34: 28-29, "Naye akaandika katika hizo mbao, hayo **maneno ya maagano hizo amri kumi** (Noti hapa: agano ni amri). Hata ikawa, Musa aliposhuka katika Mlima Sinai, **na zile mbao mbili za ushuhuda** zilikuwa mkononi mwa Musa, hapo aliposhuka katika mlima, Musa hakujua ya kuwa ngozi ya uso wake iling'aa kwa sababu amesema naye (Mungu). Ndiyo amri kumi ziliandikwa katika mawe mawili katika Mlima wa Mungu, Lakini Mungu alimwambia Musa aandike tena pamoja na sheria zote nyingine katika kitabu (chuo) kinachoitwa torati! Tusoma Kumb. 31:24-26, "Basi ikawa hapo ***Musa alipomaliza kuandika* maneno ya torati** **hii katika chuo**, hata yakaisha, ndipo Musa akawaamuru Walawi waliokuwa wakilichukua sanduka la agano la Bwana, akawaambia, Twaeni **chuo hiki cha torati**, mkiweke **kando ya sanduka la agano la Bwana**, Mungu wenu, ili kiwepo kama shahidi juu yako." Sasa tuangalia, Kut. 24:4 na 7, "Basi *Musa akayaandika maneno yote* ya Bwana.....Kisha akakitwaa ***kitabu cha agano*** akakisoma masikioni mwa watu; wakasema, hayo yote aliyoyanena Bwana tutayatenda, nasi tutatii."

Kwa hiyo tumeona kwa urahisi kwamba "Musa alipomaliza **kuandika maneno ya torati**." "Musa akayaandika maneno yote ya Bwana...kisha **akakitwaa kitabu cha agano**." Kwa hiyo maneno ambayo Musa aliandika kutoka kwa Mungu ni **TORATI NA AGANO**. Agano gani? Agano kati ya Mungu na wana Waisraeli. Torati ambayo amri kumi ziliandikwa ndani ilikuwa agano! Ndio maana ilitunzwa pamoja na sanduka la agano.

Lakini tusimalize hapa, tuangalie maneno ya Paulo katika Rum. 7:7. Mtume Paulo alisema, "Singalitambua dhambi ila kwa **sheria**, kwa kuwa singalijua kutamani, kama **torati** isingalisema, **USITAMANI.**" Sasa imeandikwa wapi kwenye torati kwamba usitamani? Imeandikwa katika Kum. 5:21, katika **amri kumi,** Amri Kumi hapa zilisema "USITAMANI". Na Paulo kupitia Roho Mtakatifu aliaandika ya kuwa, sheria=torati=usitamani=amri kumi. Paulo alisema, asingejua kuwa kutamani ni dhambi pasipo sheria ambaye aliita sheria ni torati katika mst. 7. Na tunajua kwa hakika bila kukosa na bila wasiwasi kwamba "USITAMANI" ni mojawapo ya amri kumi. Kwa hiyo Paulo alielewa kwamba torati na amri kumi ni mamoja. "Singalijua kutamani, kama **torati** isingalisema." Na "Usitamani" ni amri ya kumi katika amri kumi. Kwa hiyo tumeona kwa urahisi kupitia mafundisho ya Musa na Paulo kwamba **Torati na Agano ni kitu kimoja.**

**Sasa, kwasababu tumeshaona Amri Kumi, Agano la Kale na Torati ni kitu kimoja. Je, Tufuate Agano lipi leo?**

Turudie Biblia, tusoma 2 Kor. 3:6-8, 11-16, "Naye, (Mungu) ndiye aliyetutosheleza kuwa wahudumu wa **Agano Jipya**; si wa andiko, bali wa roho**; kwa maana andiko huua, bali roho huhuisha.** Basi, **ikiwa huduma ya mauti iliyoandikwa na kuchorwa katika mawe** (yaani, amri kumi) ilikuja katika utukufu, hata Waisraeli hawakuweza kuukazia

macho uso wa Musa, kwa sababu ya utukufu wa uso wake; nao ni utukufu uliokuwa ukibatilika; je! huduma ya roho haitazidi kuwa katika utukufu?....Kwa maana, ikiwa ile inayobatilika ilikuwa na utukufu, zaidi sana ile ikaayo ina utukufu. Basi, kwa kuwa tuna taraja la namna hii, twatumia ujasiri mwingi; nasi si kama Musa alivyotia utaji juu ya uso wake, ili kwamba Waisraeli wasitazame sana mwisho wa ile iliyokuwa ikibatilika; ila fikira zao zilitiwa uzito. Kwa maano hat leo hivi, **wakati lisomwapo Agano la Kale, utaji uo huo wakaa**; haikufunuliwa kwamba huondolewa katika Kristo; ila hata leo **torati ya Musa isimwapo, utaji huikalia mioyo yao.** Lakini, wakati wo wote watakapomgeukia Bwana, ule utaji huondolewa."

Kwa hiyo tumeona kwamba amechanganya amri kumi (zilizochorwa katika mawe, mst. 7), agano la kale (mst. 14) na torati (mst.15) katika mistari hii na kusema ni **huduma ya mauti inayobatilika**. Kwa maana katika karne ya kwanza na leo, amri kumi ni huduma ya mauti, agano la kale ni huduma ya mauti na torati ni huduma ya mauti!

Kwa hiyo leo Mungu alisema yeye mwenyewe kupitia Paulo kwamba Amri Kumi, Agano la Kale na Torati ni kitu kimoja. Na tena ni bure kwa sisi leo kwa sababu italeta **mauti!** Pia soma Yer. 31:31-32; Ebr. 8:13; Ebr. 8:6-7; Ebr. 10:4-5; Ebr. 9:15; Ebr. 10:8-9.

Leo Mungu alimtuma Bwana wetu Yesu Kristo, alisulubiwa kwa ajili ya watu wote. Na kama tunataka wakovu leo, tutaacha vitu ambavyo vilileta mauti. Na kufuata Yesu na maneno yake, "Asiyedumu katika mafundisho ya Yesu hana Mungu," 2 Yoh. 9.